

MSWADA NA 234

Mnukuzi: P. Ridhiwani

1. Leo nashika kalamu, kuzinudhumu nidhamu  
Kula asiye fahamu, yapate kumuelea
2. Wala mimi sikutaka, mambo haya kutamka  
Lakini nasononeka, kwa niliyoyasikia
3. Nami singeliyanena, ila ninayo maana  
Nachaa yasizuke tena, haya niloyasikia
4. Habari nilotolewa, ni mwendani za kuzua  
Leo nitazifunua, niukomeshe ubaya
5. La kwanza natangaziwa, ya kuwa ninadaiwa  
Na deni lanisumbuwa, nashindwa kujilipia
6. Lakini ningaambiwa, nasema singedaiwa  
Ila nimuaminiwa, singepashwa mia mia
7. Na ambaye anidai, hiwa sina sikimbii  
Humtunza kwa tumai, nipatapo humwendea
8. La pili lilotangaa, Makadara kwa jamaa  
Ni nyumba ninayokaa, silipi yanilemea
9. Lakini ningaambiwa, kuwa kodi nalipiwa  
Mimi nasema si sawa, mwenyewe najilipia
10. Nalipa ya chumba changu, na chumba cha ndugu yangu  
Hivi leo walimwengu, wanena wanilipia
11. La tatu ni la chakula, tununuwacho jumla  
Naambiwa nina ila, mwenzangu namlimia

12. Lakini mimi najibu, kuwa hayo si thawabu<sup>1</sup>  
Ni maneno ya kidhabu,<sup>2</sup> ambaye anizulia
13. Mimi kwangu nala changu, na mke na ndugu yangu  
Naatwaacho mwenzangu, ni chake ajilipia
14. Mimi kwangu sili kwake, wala sinywi maji yake  
Nala changu ala chake, silipiwi hata moya
15. Na iwapo yuwakana, maneno ninayo nena  
Na aje ana kwa ana, tunene maneno haya
16. Mimi sipendi maneno, yasiyo masikizano  
Leo huwaje hayano, mwenzangu kunizulia
17. Lakini hapana kitu, kwa waja ni ada yetu  
Yule atendae utu, kwake hulipwa mabaya
18. Nami haya kunifikia, ni Aswila alotaka  
Maana kula shirika, mimi sikupendelea
19. Na hapa nilipofika, sitaki tena shirika  
Afadhali haepuka, isinifike balaa
20. Kwani mimi sikutaka, kula chakula shirika  
Ni mwenzangu menitaka, na mimi hamridhia
21. Na lau ningalijuwa, kuwa haya yatakuwa  
Kitambo ningejivua, hawa mbali na balaa
22. Na hivi sasa wendani, siwi tena shirikani  
Tapika changu nyumbani, tusiwe chungu kimoya
23. Kwani ndiyo afadhali, kula mtu chungu mbali  
Shirika ina muhali, naichelea balaa
24. Na muda hipika changu, sitovunda ada yangu  
Tampa naye mwenzangu, na chake nitapokea
25. Wala sitakasirika, kwa aliyoyatamka  
Na nyumbani akitoka, sipunguwi hata moya
26. Alipokuwa ataka, kukaa nami shirika  
Alikuwa hamuweka, na mengi hamfanyia
27. Wala mimi sitanena, nilomtenda akhana<sup>3</sup>  
Subhana<sup>4</sup> yuwaona, ndiye wakunilipia

28. Na iwapo yatazuka, ya jamvi kulitandika  
Basi hapo tatamka, kula neno moya moya
29. Tanena pasi kufita, wala sitasitasita  
Maana sipendi vita, na maneno yaso ndia
30. Umbo langu kwa bayana, sipendi kusengenyanana  
Hupenda kuambiana, usawa ulolekea
31. Wala sichi kutamka, kwa jambo lenye hakika  
Muungwana hufunuka, hafiti lilolekea
32. Na mwenye kucha kunena, akawa husengenyanana  
Huyu hawi na maana, ni muovu wa dunia
33. Na wala hawi ni mtu, mwenye kusifia watu  
Huitwa ni nyoka satu, aumaye kivivia<sup>5</sup>
34. Nami naomba wendani, alo na neno moyoni  
Nanikabili matoni<sup>6</sup>, nasiniche kunambia
35. Na hapa nilipokoma, ndiyo mwisho wa kalima  
Rabi tanipa salama, ya akhera na dunia

#### Mwisho

---

1.	Thawabu	=	pato
2.	Kidhabu	=	mwongo
3.	Akhana	=	ndugu yetu
4.	Subhana	=	Ni neno litumikalo kwa kumsifu Mwinyiezi Mungu
5.	Vivia	=	puzia
6.	Matoni	=	machoni